



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 5th March, 2024
Third Assembly – Third Session
TENTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:38p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Have your seats Members.

[Silence]

Serjeant-At-Arms, please ring the quorum bell under Standing Order Number 31 (2).

[The Serjeant-At-Arms rung the quorum Bell]

Clerk, confirm if there is quorum!

[Quorum confirmed]

Yes, Clerk next Order please?

NOTICE OF MOTION

MEASURES TO ADDRESS SHORTAGE OF FRESH WATER IN MOMBASA COUNTY

Yes, Honourable Maryam Baimu?

Hon. Baimu: Thank you Mr. Speaker Sir. I beg to move the following Motion;

AWARE THAT, water is a fundamental human right recognized by international treaties and enshrined in Article 431(1) of the Constitution of Kenya;

FURTHER AWARE THAT, the Fourth Schedule of the Constitution assigns the County government the mandate to address water and sanitation and acknowledging the Water Act (2016) and other relevant legislation;

NOTING THAT, access to clean and sufficient water is crucial for public health, economic development, and the realization of basic human rights;

APPRECIATING the efforts of His Excellency the Governor in emphasizing the importance of water resource management;

ACKNOWLEDGING the existing shortages of fresh water in Mombasa County, affecting citizen, county buildings, and offices;

CONCERNED THAT the current situation poses a severe threat to public health, economic activities, and the overall well-being of Mombasa County residents;

DEEPLY CONCERNED THAT, despite earlier resolutions, the water shortage situation persists, exacerbating the hardships faced by the residents;

I, therefore, urge this Assembly to RESOLVE:

- 1. THAT the County government takes immediate steps to address the shortages of fresh water in Mombasa County, including county buildings and offices;*
- 2. THAT water infrastructure is upgraded and expanded to ensure a reliable and sustainable water supply;*
- 3. THAT public awareness campaigns are conducted to educate residents on water conservation and efficient water use practices;*
- 4. THAT the County government collaborates with relevant stakeholders to explore alternative water sources and technologies;*
- 5. THAT the County government allocates adequate funds to implement these measures effectively;*
- 6. THAT the relevant County departments work in coordination to streamline water management efforts;*
- 7. THAT the County government engages in partnerships with external agencies to access technical expertise and financial support for water projects.*

Thank you, Mr. Speaker Sir.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Maryam Baimu for the Notice of Motion. Yes, Clerk next Order please?

MOTIONS

ADOPTION OF THE REPORT OF THE COMMITTEE ON PROCEDURE AND RULES ON THE PROPOSED AMENDMENTS TO PART XXI OF STANDING ORDERS AND THE SECOND SCHEDULE

[Silence]

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 2*

Any Member from the Committee on Procedure and Rules, Honourable Prischillah are you a Member of Procedure and Rules Committee?

The Chief Whip (Hon. Mumba): Yes.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay proceed.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker, I beg to move the following Motion;

THAT Pursuant to Standing Order 233 (5), the Report of the Committee on Procedure and Rules on the Proposed Amendments to Part IX of the Standing Orders and Second Schedule as laid on Tuesday, 5th March, 2024 during the 9th Sitting be approved.

[Silence]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Prischillah (Shillah) please read again.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Thank you Mr. Speaker. May I repeat because there was a slip of the tongue. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

THAT Pursuant to Standing Order 233 (5), the Report of the Committee on Procedure and Rules on the Proposed Amendments to Part XXI of the Standing Orders and Second Schedule as laid on Tuesday, 5th March, 2024 during the 9th Sitting be approved.

I beg Honourable Morgan as a Member to second.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Morgan?

Hon. Matsaki: I beg to second.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now propose a question that the Motion on Adoption of the Report of the Committee on Procedure and Rules on the Proposed Amendments to Part XXI of Standing Orders and the Second Schedule be debated in this House?

[Question proposed and agreed to]

Yes, Leader of Majority any input, sorry the Chief Whip?

The Chief Whip (Hon. Mumba): Mr. Speaker Sir, because Members have a copy, I do not have to read everything that is in the copy I think am I my right or wrong? Do you have the copy? So...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Prischillah (Shillah) just build on your Motion instead of reading the Report; just build on your Motion?

The Chief Whip (Hon. Mumba): Mr. Speaker Sir, Section 14 of the County Government Act 2012 provides that; A County Assembly; -

(a) *May make the Standing Orders consistent with the Constitution and this Act regulating the procedure of the County Assembly including, in particular, orders for the proper conduct of proceedings; “and,*

(b) *Subject to Standing Orders made under paragraph (a), may establish Committees in such manner and for such general or special purposes as it considers fit, and regulate the procedure of any Committee so established”.*

Mr. Speaker, further Standing Order No. 187 of the Mombasa County Assembly Standing Orders establishes the Select Committee on Procedures and Rules with its mandate being inter-alia; -

i. *To consider and report on all matters relating to the Assembly Standing Orders;*

ii. *Propose amendments to the Assembly Standing Orders and any such amendments which shall upon approval by the County Assembly, take effect at the time appointed by the County Assembly, and,*

iii. *Propose rules for the orderly and effective conduct of Committee Business and any such rules, which shall upon approval by the County Assembly, continue in force until amended or repealed by the County Assembly.*

Mr. Speaker, I beg to stop because they have the following Report. Thank you, Mr. Speaker Sir.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali ya yote kwanza nishukuru ofisi yako na ya Katibu, lakini zaidi nishukuru Kamati yako iliyokuwa na dhima ya kusimamia suala hii ambalo leo tumebahatika kupata Ripoti hii. Mheshimiwa Spika, binafsi ni chanzo cha mchakato huu wa mapendekezo ya mabadiliko katika Kanuni zetu za Kudumu na nishukuru katika vikao ambavyo Kamati yako ilikaa kwa wakati maalum ilikuwa ni kihusishwa kwa kualikwa vikao vile na kuchangiza ama kuhoji na kuhojiwa. Vile vile pale ambapo ilikuwa nimeathamirika katika yale mapendekezo, miongoni mwa yale mapendekezo Mheshimiwa Spika ambayo Kamati yako yaliyaafiki ya kwanza ni marekebisho ya kipengele cha 157 cha Kanuni zetu za Kudumu ambacho kimepeana fursa Kamati ya Uteuzi katika kupangilia Kamati ziwe katika namba isiyogawanyika kwa mbili na nambari hii isiwe chini ya saba, tisa na isiwe zaidi ya wanachama kumi na mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati tulizokuwa nazo awali zilikuwa na chini ya saba na si zaidi ya tisa na ikawa ina uhaba wa uwakilishaji na wakati mwengine kama utakuwa na wawakilishi katika Kamati inavyostahiki lakini hivi sasa Kamati zetu zitakuwa na mseto unaostahiki kwa sababu idadi itasonga kutoka tisa hadi idadi ya kumi na moja. Mheshimiwa Spika, vile vile katika sehemu ya 187 tumeondoa neno *Accounts* ama *Uhasibu* na kuweka *Uwekezaji*; hivyo kupeana fursa ya kuwa sasa hivi kutakuwa na *Kamati ya Uwekezaji ya Mali ya Umma* na *Kamati ya Uhasibu* ambazo zitakuwa ni Kamati mbili. Mheshimiwa Spika, pia kwa haraka haraka tumeweza kupeana nafasi katika Kanuni zetu za kudumu kuundwa Kamati maalum ya kusimamia mamlaka na fursa zetu katika Bunge hili ambalo ni letu sisi Wawakilishi. Mheshimiwa Spika, lakini pia vile vile italinda haki za wafanyikazi wetu kwa sababu wakati mwengine mfanyikazi anaweza kuhujumiwa na Mheshimiwa na pengine akakosa mahali pa kufikisha suala hili ama changamoto hii kwa inavyostahiki.

Kwa hivyo pia Kanuni zetu za Kudumu pia zimeweza kupeana fursa ya Kamati hii ya Mamlaka na Fursa. Mheshimiwa Spika, Kamati nyengine ambayo imeweza kupewa fursa katika Kamati hii ambayo tunajadili leo ni ya Usimamizi wa Masuala ya Usalama na Majanga. Katika Ibara ya nne ama ratiba ya nne ya Katiba yetu miongoni mwa Kanuni ama miongoni mwa majukumu tuliopewa kama Gatuzi ni usimamizi wa wazima moto na majanga. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika Kamati hii ina umuhimu kwa sababu ni majuzi tumekuwa na majanga lakini wakati mwengine tunakosa Kamati katika Bunge ambalo litachukua dhamana ya kufuatilia ama kusaraangi upande wa pili kwa sababu pia katika suala la majanga kuna asilimia moja ya bajeti yetu ya Gatuzi kuwekwa katika haya masuala ya majanga Mheshimiwa Spika. Vile vile Mheshimiwa Spika tuna *Kamati ya Fursa za Usawa* ambayo Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kiutamaduni huwa inapeana nafasi kwa watu wetu waliobaguliwa ama wanahisi kubaguliwa; miongoni mwao ni walemavu, ni vijana, ni kina mama kwa hivyo Kamati hii mwisho wa siku utaona imeshimiri vitengo vinavyostahili ambavyo vitakuweko na fursa ya kuangazia yale ya dhulma, yale ya ubaguzi katika Kaunti yetu ili tuweze kuwa mfano mwema wa kuigwa. Na katika mapendekezo yake vile vile Mwakilishi wa Walemavu ndio atabahatika kuwa katika fursa ya Kamati hii. Pia Kamati ya Masuala ya Elimu Mheshimiwa Spika kama ilivyo katika ratiba ya nne tumepewa fursa ya kusimamia Elimu ya Chekechea, Vyuo Anuwai na kadhalika lakini kwa mujibu wa sheria zetu vitu ambazo tulipitisha katika Jumba hili tuliweza kupeana fursa ya kwamba Serikali itaweza kusimamia baadhi ya shughuli za Kielimu ikiwemo Mheshimiwa suala la basari, suala la mikopo kwa wanafunzi lakini vile vile Mheshimiwa Spika suala la kuwalisha wanafunzi wetu wa chekechea katika shule zetu ili tuweze kutekeleza hilo tumeweza kuigawanya Kamati hii kuwekeza katika masuala ya Elimu, Masuala ya Chekechea, Vyuo Anuwai na shughuli za Kielimu kando lakini pia tukaja na Kamati ambayo itasimamia masuala ya kiteknolojia na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pia baadhi ya Kamati katika mipangilio ya ratiba yetu katika Kanuni za Kudumu zilikosa majina yanavyostahiki na pia nishukuru ya kwamba Kamati yako imeweza kuangazia na huku katika Ripoti pia zimeweza kutajwa kwa ruhsa yako nitanukuu kama zilizavyo, *Blue Economy, Livestock, Agriculture and Cooperatives, Environment, Waste Management and Energy, Water, Natural Resources and Climate Change Resilience, Health Services, Youth, Gender, Sport and Social Services, Transport and Infrastructure, Trade, Tourism and Culture, Early Childhood Development and Educational Programmes, Labour and Public Administration, Lands, Housing and Urban Planning, Justice and Legal Affairs and Committee on ICT and Digital Transformation*. Kwa hayo Mheshimiwa Spika ni naunga mkono Hoja hii na naomba Waheshimiwa Wenza waweze kuunga mkono tuweze kwenda sambamba na shughuli zetu katika mipangilio ya Kamati. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Matsaki?

The Leader of Minority (Hon. Matsaki): Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nasimama mbele ya Waheshimiwa wenza kuunga mkono kwa sababu jambo la kwanza, awali Kamati mwanzo zilikua ni chache lakini hivi zimezidi kuongeza hizi Kamati hivo ni kwamba kila mmoja ataweza kuonekana kila kamati kwa hivyo Mheshimiwa Spika wacha nishkuru kwanza wahasika walioweza kuchukua hatua hii na kuwapongeza. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu): Thank you yes Honourable Frankline Makanga.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa mwenyekiti na mimi pia nasimama kuunga mkono hoja hii ambayo imeweza kuletwa kwetu na Kamati iliyohusika na pia vilevile nipongeze juhudi za wote waliohusika wakiwemo upande wa ukatibu ukiongozwa na katibu mkuu ambae ni *Clerk* wetu wa Bunge hili na vilevile nishukuru ofisi yako Mheshimiwa Spika kwamba mumeweza kuangazia kati ya matakwa mengi yale ambayo ni majukumu yetu ya kikatiba kulingana na katiba ya mwaka, 2010 sehemu ya nne ama the *Fourth Schedule*. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ukiangalia kati ya mambo mengi ambayo yameweza kufanyika hapa ikiwemo kuweza kugawanywa kwa Kamati ambayo inaangazia maswala ya *County Public Investments Committee*, pamoja na *Public Accounts Committee*, Mheshimiwa Spika hii ni ishara kwamba na dhahiri kwamba ipo kazi ya Bunge hili kufanya kazi yake inavyostahiki na katika kuweza kufanya hivi ninaamini Bunge hili litakua na wakati mzuri kupitia Kamati hizi kuweza kuangalia kila kinachoingia kwani serikali ya Mombasa na kile kinachotoka kwa njia inayostahili kwa kuzingatia kanuni na sheria na katiba ya Kenya. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ninaamini Kamati hizi zote zimeweza kuletwa katika Bunge hili zitaweza kufanya kazi yake, zitaweza kuangalia mipangilio inayostahili na hivyo hivyo katika taarifa hii ambayo tulioletewa imeweza pia kuonyesha majukumu ambayo Kamati hizi itafanya lakini naamini kwamba sisi sote ambao tuko katika Bunge hili lengo letu na nia yetu ni kuwafanyia haki wakaazi wa Mombasa, kuwafanyia haki kwa kuwawakilisha na kuwafanyia haki kwa kuwa sauti yao tuwe wasemaji wa wananchi pale mashinani. Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mimi nasimama kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Madialo.

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker Sir. I would like to invite the Honourable Members to come with me and look at page number ten, now number five that a new Standing Order be inserted to establish a Committee to be known as a Committee on County Security and Disaster Management so as to read as follows blah blah blah to the end. Now when you go to the pages behind where the Committees are inserted that Committee has not been inserted, I would also like to ask a rhetorical question; this Committee that is being formed I understand that it has been hived from the committee on Labor and Public Service Administration because disaster was domiciled at the public service administration having said so I am in support. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Abdulrahman.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Thank you Honourable Speaker. I'm still going through the document however I have no objections and I will still take my time to go through it thank Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Nyota.

Hon. Hamisi Nyota: Thank you Honourable Speaker for giving me this opportunity to make my contribution. Honourable Speaker, I stand to support this Motion and mostly give much congratulations to the Committee which came up with this Report; the introduction of the new Committee not only enriches our Standing orders but also give us maximum opportunity to do our oversight role effectively and efficiently. Honourable Speaker, I think its high time that we should pick up our roles well and ensure that the residents of Mombasa get the maximum benefit from this House. Thank you so much Honourable Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, thank you. Yes, Honourable Mwaka.

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii nami niweze kuweka sauti yangu hapa. Mimi nasimama kuunga mkono Kamati hii ilivyoongeza hizi Kamati, kwa kusema kweli Kamati zilikuwa ni chache na ambazo kwamba zimebebebwashwa majukumu ambao kwamba mengine ni mengi, nikiona kama hapa kwenye *Security and disaster* mara nyingi sana hii ilikuwa ikilemezewa kwa upande wa usafiri kwa sababu imeoana na hino *disaster*. Hapo kama kutakua na Kamati yake peke yake itakua imepunguza uzito, mimi nasimama kuipongeza na kuwapongeza waliokaa wakabuni hizi Kamati vile vile pia kuongezea ile idadi ya Kamati ili tuweze kufanya kazi na pia wengine nao wapate majukumu ya kuweza kufanya kazi Kamati. Ni hayo tu Mheshimiwa Spika, ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Katana.

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity though I was not prepared to comment anything on this. Citing Standing Order 179(7) which says, *within 48hours after the Report has been laid on the Table of the County Assembly the Clerk shall publish the Report in the County Assembly website and circulate copies to Members* the reason saying that I would reserve my comments Mr. Speaker on this, it is because I have not gotten proper time go through the Report and maybe because it may be a routine I then beg to support. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Kai.

Hon. Kai: Thank you, Mr. Speaker. I do support.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu): Thank you I now call upon the mover of the Motion to reply.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama hapa tena kuunga mkono kwa wale wote wameunga mkono Mswada huu; Mswada huu umekuja kwa nia njema kwa sababu katika Jumba hili kama tunavyojua, tulikuwako na zile Kamati tulizonazo ni kidogo na kuna Kamati ambazo zilikuwa hazijaguswa ambazo zilikuwako zinahitaki kujumuishwa manake tulikuwa tunapata Ripoti kutoka mashinani lakini tulikuwa hatujui tupeleke haya majukumu kwenye Kamati gani.

Pili, kama vile Mheshimiwa mmoja alivyosema hapo Mheshimiwa Mwaka kuna majukumu mengine yalikua yanaoana katika wizara mbili ambapo inakua uzito kwa Mwenyekiti ambae ni wa hiyo Kamati hajui atagawanya yale majukumu kiviipi. Kwa hivyo ilikua imetufanya tuweze kupanua hizi Kamati ndio majukumu yaweze kuwa rahisi kwa Wenyekiti mbali mbali ambao wanasimamia hizi Kamati na waweze kuwa na urahisishaji wa kazi zao na pia katika viongozi wale tuko nao hapa kuna wale ambao walikua wako nyuma na Kamati walikua Kamati zao ni kidogo na unakuta mtu ana Kamati kama mbili wengine wana Kamati nne na mwingine ana Kamati tatu, na mwengine ana Kamati moja. Kwa hivyo ikawa kidogo unaleta msukamano hapa kuona kama kuna tofauti, lakini kwa sasa tumejaribu kadri tunavyoweza tutengeze Kamati ambazo zitahusisha Waheshimiwa wote kwa jumla, wawe na majukumu ya Kamati zaidi ya tatu kwa kila kiongozi. Na ningependa kusema, taarifa itakapokuja nafikiri kizungu mimi si lugha yangu sana lakini imetumiwa ni *shall* ama ni *may*. Kwa hivyo ikiwa imetumika neno hilo, ikiwa ni dakika kumi, ishirini, hamsini ama lisaa limoja, mimi sioni kama kuna tatizo kwa muda ule ambao tumepeana nakala hizi, ilikuwa ni mda ambao ni mwafaka wa kuangalia na kwanza, nyingi ni Kamati ambazo ziko zinazofanya kazi. Kwa hivyo kama ni Kamati mpya nafikiri ni mbili ama tatu ambazo ndio zimeongezeka na haikuleta taarifa ndefu ya kusema itahitaji siku mbili ama tatu kwa Mheshimiwa kuelewa, maana kuongeza Kamati mbili ama moja katika nakala hii kuwa itatamausha. Kwa hivyo ninawashukuru Waheshimiwa wote wacha tupitishe nakala hii, ndio tuweze kuweka hizi Kamati tuanze kufanyia watu wa Mombasa kazi. Ahsanteni.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now stand to put a question that the Motion on Adoption of the Report of the Committee on Procedure and Rules be approved by this Honourable House?

[Question put and agreed to]
[Applause]

Yes Clerk?

PROMOTION OF USAGE OF KISWAHILI IN THE COUNTY ASSEMBLY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT Kiswahili is one of the official languages of Kenya, as well as a lingua franca in East and Central Africa, spoken by over 200 million people, and that it is also recognized as an official language by the African Union, the Southern African Development Community, and the East African Community;

FURTHER AWARE THAT Kiswahili reflects our cultural identity and nation cohesion, as enshrined in the Constitution of Kenya, which declares Kiswahili as the national language and one of the official languages alongside English, and also mandates the State to promote and promote the development and use of indigenous languages, Kenyan Sign

Language, Braille and other communication formats and technologies accessible to persons with disabilities;

RECOGNIZING the importance of linguistic diversity and the need to foster the use of Kiswahili within our County Assembly, as a means of promoting inclusivity, accessibility, and human rights;

NOTING THAT English currently dominates as the main medium of communication in our County Assembly, despite being an official language, and that only 5 per cent of the population surveyed in Kenya spoke English as the primary language at home in 2021;

BELIEVING THAT Kiswahili can enhance effective communication and inclusivity among Assembly members and staff, as it is spoken by over 25 per cent of the population;

CELEBRATING the rich history and heritage of Kiswahili, influenced by various languages and cultures, such as Arabic, Portuguese, English German, Persian, and Bantu;

ALARMED by the potential loss of cultural and linguistic identity if proactive measures are not taken to promote Kiswahili within the assembly;

AWARE THAT Kiswahili is one of the official languages of Kenya, as well as a lingua franca in East and Central Africa, spoken by over 200 million people, and that it is also recognized as an official language by the African Union, Southern African Development Community, and the East African Community;

I, therefore, urge this Assembly to RESOLVE:

- 1. THAT, the County Assembly actively promotes and encourages the use of Kiswahili in debates, discussions, and official communications;*
- 2. THAT, the County Assembly facilitates Kiswahili language training for Assembly Members and staff, improving their proficiency in both spoken and written Kiswahili;*
- 3. THAT, the County Assembly incorporates Kiswahili translations in official documents, including agendas and minutes, to ensure accessibility inclusivity;*
- 4. THAT, the County Assembly establishes a weekly plenary sitting every Wednesday morning, dedicated to debate and communications conducted exclusively in Kiswahili, as a proactive measure to enhance the practical application and proficiency of the language among Assembly Members.*

May I, ask Honourable Hassan Mohammed to second the Motion.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Hassan Mohammed?

Hon. Hassan Mohammed: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa vile vile na kuweza kuunga huu mjadala ambao umeweza kuletwa.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Are you seconding or?

Hon. Hassan Mohammed: Si naunga ama mwataka nikatae pia?

[Consultations]

[Laughter]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay Honourable Members, I now propose a question that the Motion of usage of Kiswahili in the County Assembly be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Athman Rama, the Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika tutakubaliana ya kwamba kuna taifa limeweza kusonga pasi kuitambua historia yao. Tunapokuja katika sanaa Mheshimiwa Spika miongoni mwa nyenzo za sanaa ni utumizi ya lugha, watu hutambulika kwa lugha yao. Mheshimiwa Spika kwa hoja hii, inalenga utamaduni wetu na fursa ya sisi kutambulika katika dunia nzima ya kwamba asili ya lugha hii teule ambayo sasa inatumika na zaidi ya watu milioni 200 na asili yake ni Mombasa na kwetu sisi kuitunza, ni heshima kwetu na kwetu sisi kuitunza tunapeana fursa hata kwa mataifa wengine hususan wanaofunza lugha hii ya Kiswahili katika vyeo vyao kama Amerika, Finland na kadhalika kupata sababu ya kuzuru mji huu wa Mombasa na kuhudhuria baadhi ya vikao vyetu vya Bunge. Kama ilivyoratibiwa ya kwamba Bunge likiafiki siku ya Jumatano asubuhi iwe ni siku maalum ya kuchangia Miswada yote na shughuli zote za Bunge kwa lugha ya Kiswahili, tutapata wageni mkuki katika siku hio kuja na wao kujifunza ueledi wa lugha hii inayozungumzwa Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, mimi nishukuru ya kwamba Bunge hili linawatashi katika matumizi ya lugha hii ya Kiswahili na wale wachache ambao kwa bahati mbaya wana ulimi mzito kama ndugu yangu...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Fatma converse in low tones. Let us proceed.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Kama ndugu yangu Mheshimiwa Spika nitampa fursa kwa sababu hii itamjengea nafasi ya uaminifu zaidi kwa watu wake, kwa sababu atakuweko na uwezo wa kuchangia ama kujibizana ama kuelezana na watu wake kwa lugha pendwa, ama lugha ya mama ya maeneo yetu haya ya Mombasa. Kwa hayo mengi Mheshimiwa Spika niwaombe tu Waheshimiwa wenza ya kwamba, asili yetu, utamaduni wetu na kutambulika kwetu awe ni lugha ya mama na lugha ya mama kwetu sisi, ni lugha ya Kiswahili ambayo sasa hivi ni lugha ya kitaifa tunashukuru kwa heshima hio na pia ni lugha ya kimataifa tunashukuru zaidi kwa kuheshimika katika dunia hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Nusura?

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Shuhudia?

Hon. Shuhudia Abdallah: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono mia fil mia kwa sababu, kizungu si mdomo changu kwa hivyo nimefurahi sana...

[Applause]

Kwa sababu nimesikia Kiongozi wa Wengi akisema kila Jumatano tutakuwa tukizungumza Kiswahili kwa hivyo ni furaha sana kwangu, nimeunga mkono mia fil mia. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Chief Whip?

The Majority Chief Whip (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi nimesimama hapa kuunga mkono maana lugha ya Kiswahili ni lugha yenye uwepesi katika midomo yetu, sababu wajua hapa huwa tuko na kizungu lakini leo nimemwambia hata usijaribu kupinga kitu hapa, manake hutapata kura hapa. Sisi sote tunaunga mkono Kiswahili na tunaunga Kiswahili kizungumzwe hapa na siku hizo zengine kama kutakuwa na kimombo kama tunaweka siku tano za Kiswahili, kimombo iwe siku moja. Kwa hivyo mimi niko hapa kuunga mkono na kuwarahi wenzangu, manake nafikiri Kiswahili hata ukizungumza maneno yanashuka tu kiurahisi, lakini tukizungumza hichi kimombo saa zengine unaweza sema *shall, went au when*, maneno yanapishana pishana tu manake hatukuzoea mdomoni mwetu lakini hiki Kiswahili utajitafsiri katika Bunge vizuri na watu wataweza kukuelewa na watu wataelewa hoja yako kwa ufasaha na utaweza kuungwa mkono ama kupingwa kwa sababu watu watakuwa wameelewa kwa undani kile utakacho kieleza kwa hivyo Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono mia kwa mia.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Honourable Leila?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa ruhusa ya kuweza kuchangia hoja hii. Kwanza nampongeza mwenye ambaye amekuja na hoja hii Mheshimiwa Fadhili Makarani ambaye ndie aliyeleta hoja hii katika Bunge hili. Kwa kweli amekaa akafikiria sana, kwa sababu kizungu kina wenyewe kabisa na sisi chetu ni Kiswahili mpaka tujivunie lugha yetu na Kiswahili ni lugha ya taifa na tukikuze Kiswahili kwa sababu ndicho chepesi kama vile Bi Kiranja wa Bunge amesema pale, kina wepesi wa kuweza kuongea hata na wenzako, hata kutoa hoja zako, unatoa bila wasiwasi. Kwa hivyo kidogo kizungu huwa kinatuchenga lakini vile mumetuletea hii hoja ya Kiswahi mumefanya mambo mazuri sana. Ndio sote tumesoma lakini kizungu saa zengine chatukanganya sana. Kwa hivyo mimi nashukuru sana...

[Interruption]

Mheshimiwa Spika, nilinde hapa na Kushe! Kushe ananitaziza asema niseme *I love you* kwa lazima hapa, haya sasa *I love you* yaingia wapi hapa?

[Laughter]

Mheshimiwa Spika, pia nina mwalimu wangu wa kizungu ambaye ni Mheshimiwa Milka alinifunza sana kiingereza lakini bado pia hivyo hivyo naona Kiswahili ni zaidi.

Kwa hivyo Mwalimu wangu nakushukuru kwa kuweza kunifundisha kiingereza lakini nakwambia leo tuunge mkono Kiswahili maana yake ndio lugha ambayo inakuwa rahisi kuzungumza. Ahsante sana Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante sana Bwana Spika. Pia mimi nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii ya kwamba tutakuwa tukitenga siku moja angalau kwa wiki ili tukapate kujadiliana kwa Kiswahili na tukianza mjadala kwa Kiswahili ningependa ya kwamba Bwana Spika uwe unatuelewa. Wengine wetu ambao wanatoka kule mkoa wa magharibi kuna maneno mengine ya Kiswahili ambayo yanaweza kutukanganya, kuna maneno mengine ambayo hatuwezi kuwa tunayajua kwa Kiswahili. K kwa hivyo tunapozidi kuendelea kuongea utatuelewa kwa mfano, maneno kama *Madam Commissioner*, kama baado ni ngumu kwa Kiswahili utakuwa tu unatuelewa na tutajua tukiendelea. Ahsante na naunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you, I now call upon. Yes, Honourable Fatma I wanted to call the mover of the Motion to reply but you can proceed.

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti Kwa kuweza kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingi na ardhi pasi na kizuizi kwa hapa siku ya leo ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Fadhili ikazungumzwa na Mheshimiwa Mwamwiri. Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono mia fil mia...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): What is it Chief Whip? Are you up on a Standing order? Okay have your seat Honourable Fatma.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Mheshimiwa Spika natumia hapa fursa hii kutumia lugha ya Kiswahili ndio watu watuelewe vizuri hili ni Jumba la heshima na ni Jumba linalostahili heshima zake. Wakati tunapoweka miwani juu ya kichwa, kesho miwani itakuja kuwekwa kwenye kiunoni ama itakuja kuwekwa kwenye mgongo na sio heshima katika Jumba hili, kuwa unakuwa na mavazi ya kihunihuni, yani mavazi ya kimitaani na hili ni Jumba la heshima. Nasimama kama kiranja wa Bunge maana yake nimeangalia tabia za Waheshimiwa wengine, haswa aliyekuwa akitengeneza hoja yake nimetamaushwa na kukuta miwani hata ilikuwa yaelekea kishogoni na hali ni Mheshimiwa, hatujui ni miwani ya daktari ama ni miwani ya starehe Mheshimiwa Spika, tunahitaji mavazi kamili ya Jumba hili.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Chief Whip, you can proceed Honourable Fatma.

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kabla sijazungumza, Mheshimiwa ningependa kumueleza....

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Just proceed with your Motion.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Itakuwa si haki kwa sababu amenitaja. Mheshimiwa itakuwa ni hujuma mimi kutajwa kwamba ni muhuni! Mheshimiwa, mimi si muhuni, nimeambiwa mimi ni muhuni Mheshimiwa.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Fatma, just proceed with building your Motion.

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante Mheshimiwa. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuweza kunipa fursa hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nimesimama kidete kuunga mkono kwa sababu sisi Waheshimiwa wengi hatuzungumzi Kiswahili sanifu, pia vile vile ningekuomba kama pia tunaweza kuweza kwenda kufundishwa Kiswahili sanifu...

[Applause]

Maanake katika sisi sote, ambaye anazungumza Kiswahili sanifu ni Mheshimiwa Mwamwiri peke yake! Kama kuna mtu yeyote anapinga hapa aweze kusema sisi wenyewe Waheshimiwa hapa tunakiganza ganza Kiswahili Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti iko haja ya sisi Waheshimiwa kwenda kufundishwa Kiswahili na nakuomba Bwana Mwenyekiti kwa heshima na taadhima uweze kutupatia fursa hii ya kwenda kusoma Kiswahili na Kiswahili sanifu ama Kiswahili kisafi, kinazungumzwa hapa nchini jirani tu hapa, ukivuka feri tu hapa Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia Ukunda ukivuka boda Tanzania. Mheshimiwa Mwenyekiti ndugu zetu wakisimama kwenye Bunge lao la kitaifa la Tanzania Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wewe mwenyewe unasikia burudani yaani unawatamani vile ambavyo wanaongea! Sisi Kiswahili chetu ni cha mthuzi na nini Mheshimiwa Mwenyekiti hatujui Kiswahili ikiwa mimi ni mmoja wapo! Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti mimi naunga hoja hii mkono lakini iko haja ya sisi kuenda kusoma Kiswahili. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Leader of Majority, please reply to your Motion.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, nishukuru tu Waheshimiwa wenza kuweza kuunga mkono hoja hii lakini pia katika kuchangia kwao imeashiria yale mahaba waliyo nayo katika matumizi ya lugha hii teule, lugha yetu ya Kiswahili. Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ni lugha rahisi ambayo imegawanyika katika sehemu mbili; inazo irabu na konsonanti na katika irabu kuwakumbusha tu kwa sababu ni vitu wanavifahamu, tuko na a, e, i, o, u. Hizi Mheshimiwa Spika, hutamkwa kwa kuzingatia vitu vitatu, ile (i) na (e) hutamkwa kwa sehemu ya mbele ya ulimi, (a) hutamkiwa kwa katika ya ulimi na u na o hutamkwa kwa kuuviringa mdomo lazima uwe kama wa samaki. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nimeshukuru kwamba Waheshimiwa wameomba fursa na katika pia maombi ya hoja hii kuna nafasi ya kwamba mara kwa mara Waheshimiwa tunapata fursa ya kupitia na kujifunza lugha hii si Waheshimiwa peke yake lakini pia Makarani wetu kwa sababu mwisho wa siku tumesema nukuu zote iwe zitafanywa katika lugha mbili, ya Kiingereza na ya Kiswahili. Hapo kwa kunukuu Mheshimiwa Spika kwa wafanyikazi wetu wakikosa fursa hii ya masomo ya lugha hii tutaandikiwa vitu ambavyo hatuvijui maana yake. Kwa sababu mara kumi afadhali Waheshimiwa wana lugha, lugha ya Kiswahili lakini kwa upande wa pili wa maafisa wetu Mheshimiwa Spika, tunashukuru ya kwamba wamebobeza zaidi kwa lugha ya King'eng'e.

Kwa hivyo hawa zaidi pia wakipata fiursa hii ya kusoma pamoja na Waheshimiwa itapendeza ili tuweze kwenda nao sambamba katika haya ambayo tunapangia Mheshimiwa Spika. Tunashukuru Waheshimiwa wenza na nikushukuru Mheshimiwa Spika kwa kupeana nafasi ya hoja hii katika Nyumba yako hii tukufu na niwasisitize Waheshimiwa ya kwamba hii kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu itapita, baada ya hapa lakini zaidi lazima tuitendee haki kwa kuitumia lugha yetu mara kwa mara. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Leader of Majority. Honourable Members, I now stand to put a question on promotion of usage of Kiswahili in the County Assembly to be approved in this Honourable House?

[Question put and agreed to]

ADJOURNMENT

Yes Clerk?

The House rose at 3:38p.m.